TANGAZO LA SERIKALI NA. 898 la tarehe 01/11/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1)*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA SABASABA YA MWAKA 2024

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa katika Eneo la Sabasaba ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango katika Eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Jiji Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

MIPAKA YA ENEO LA URASIMISHAJI

Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SAB1 yenye majira – nukta 804382.00MS, 9294924.00KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa KS160MG kwa umbali wa kilomita 2.9 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SAB2 yenye majira – nukta 803552.00MS, 9292176.00KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa KS680MG kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi

kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SAB3 yenye majira – nukta 803385.00MS, 9292110.00KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini -Mashariki katika uelekeo wa KZ030MS kwa umbali wa kilomita 1.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SAB4 yenye majira – nukta 803494.00MS, 9293690KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa KZ070MS kwa umbali wa kilomita 1.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SAB5 yenye majira – nukta 803645.00MS, 9294827.00KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeowa KZ070MS kwa umbali wa kilomita 1.15 hadi ulipoanzia.

Dodoma,
28 Oktoba, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*